# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***29 Juni, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
## SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemtumia salamu za rambirambi Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Nurdin Hassan Babu kufuatia vifo vya watu 38 vilivyotokana na ajali ya barabarani iliyotokea tarehe 28 Juni, 2025 majira ya saa 11 jioni katika eneo la Sabasaba, Wilaya ya Same, mkoani humo.

Ajali hiyo imehusisha basi la abiria aina ya Fuso lenye namba za usajili T 179 CWL, mali ya Kampuni ya Channel One na gari aina ya Mitsubishi Rosa lenye namba T 199 EFX, mali ya Kampuni ya Mwani, baada ya basi hilo kupasuka tairi na kupoteza mwelekeo kuelekea upande wa pili wa barabara, kugongana uso kwa uso na Mitsubishi Rosa na kusababisha magari yote kuteketea kwa moto.

Katika ajali hiyo, watu 38 wamefariki dunia, wakiwemo wanawake wawili, huku miili 36 ikiwa haitambuliki kutokana na majeraha ya moto. Aidha, watu 28 wamejeruhiwa (wanawake 15 na wanaume 13). Majeruhi 22 wameruhusiwa kurejea nyumbani baada ya kupata ahueni kufuatia matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Same.

Majeruhi sita (wanaume watano na mwanamke mmoja) wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Same, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mawenzi na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC. Aidha, miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Same (miili mitano) na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC (miili 33)

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Uongozi wa Mkoa umechukua vinasaba vya miili ya marehemu na kuviwasilisha katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya KCMC, Moshi ili kusaidia utambuzi wa miili hiyo na kurahisisha taratibu za maziko kwa ndugu na familia zao.

Rais Dkt. Samia anatoa wito kwa madereva wote nchini kuzingatia umakini na kufuata sheria za usalama barabarani.

Vilevile, Rais Dkt. Samia anawapa pole wafiwa wote na anaungana na familia za marehemu na wote walioguswa na msiba huu mkubwa katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Mwenyezi Mungu awape majeruhi nafuu ya haraka na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu